

LINARUDIWA, TANGAZO LA KAZI

Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania



Wizara ya Maji
Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini



**TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI KATIKA MIRADI YA MAJI VIJIJI VYA
WILIKO, IRINGA MVUMI, MAKANG'WA, MVUMI
MISSION, NG'HAMBAKU, IKOMBOLINGA, MGUNGA, CHANHUMBA, ZAJILWA, SOLOWU,
KWAHEMU, IKOMBO, MLOWA BWAWANI, SEGALA NA CHIFUKULO**

**WAKALA WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA VIJJINI (RUWASA) WILAYA YA
CHAMWINO KWA NIABA YA JUMUIYA ZA WATUMIA MAJI NGAZI YA JAMII VIJIJI
HUSIKA INAWATANGAZIA NAFASI ZA KAZI ZIFUATAZO:-**

1. MSIMAMIZI WA JUMUIYA/FUNDI WA MRADI - NAFASI (15)

SIFA ZA MUOMBAJI:

- i. Awe na Cheti cha Fundi Sanifu Maji grade one, two, three au Diploma na kuendelea.
- ii. Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu kwenye kazi za miradi ya maji.
- iii. Awe na uwezo wa kufanya kazi pamoja na kuwasimamia mafundi wasaidizi
- iv. Awe na Umri kuanzia miaka 18-45
- v. Awe raia wa Tanzania
- vi. Awe tayari kufanya kazi pasipo kusimamiwa
- vii. Awe Mwaminifu na Mwadilifu na asiwe amewahi kufungwa jela

MAJUKUMU YA MSIMAMIZI WA JUMUIYA ZA MAJI:

- i. Atakuwa ndiye Msimamizi Mkuu wa Jumuiya ya Watumia Maji katika ngazi ya Jamii na Katibu wa Jumuiya ya watumia Maji.
- ii. Kusimamia, kutekeleza na kufuutilia shughuli zote za uendeshaji wa mradi wa Maji katika eneo husika.
- iii. Kusimamia ukusanyaji wa Ankara za maji na kutunza nyaraka zote za shughuli za uendeshaji wa mradi
- iv. Kusimamia utoaji wa Maji yenyе ubora yanafika kwa wateja/wananchi.
- v. Kuandaa taarifa za uendeshaji za mradi mfano: Mapato na Matumizi na kuwasilisha kwa Jumuiya ya Watumia Maji na Meneja RUWASA Wilaya.
- vi. Kuandaa taarifa za utekelezaji wa shughuli za mradi za Mwezi, Robo na Mwaka na kuziwasilisha kwa Jumuiya ya watumia Maji na Meneja RUWASA Wilaya.
- vii. Kusimamia matengenezo na upanuzi wa mradi na kutoa ushauri wa kiufundi kwa Meneja RUWASA Wilaya
- viii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Mradi.
- ix. Kuhamasisha uchangiaji wa huduma ya Maji, kutatua na kusuluhisha Migogoro baina ya Mteja/Mwananchi na Jumuiya.
- x. Awe tayari kufanya kazi nyingine atakazo pangwa na Meneja wa RUWASA Wilaya.

2. MHASIBU WA JUMUIYA - NAFASI (15)

SIFA ZA MUOMBAJI:

- i. Awe amehitimu masomo ya fani ya uhasibu daraja la III na kuendelea.
- ii. Awe na uzoefu usiopungua miaka mitatu kwenye kazi za Uhasibu.
- iii. Awe na Umri kuanzia miaka 18-45
- iv. Awe na ujuzi wa kutumia Komputa
- v. Awe raia wa Tanzania .
- vi. Awe tayari kufanya kazi pasipo kusimamiwa
- vii. Awe Mwaminifu na Mwadilifu na asiwe amewahi kufungwa jela

MAJUKUMU YAMHAZIBU WA JUMUIYA ZA MAJI:

- i. Atakuwa ndiye Msimamizi wa maswala yote ya Kifedha katika Jumuiya ya Watumia Maji
- ii. Kusimamia ukusanyaji wa malipo ya Ankara za maji .
- iii. Kuandaa bajeti ya mwaka ya Jumuiya ya Watumia Maji.
- iv. Kuandaa taarifa zote za fedha na kuziwasilisha kwa Msimamizi wa Jumuiya.
- v. Kufanya malipo baada ya kuidhinishwa na Msimamizi wa Jumuiya na Meneja wa RUWASA wilaya
- vi. Kutunza Vitabu vya fedha, hati za malipo na ankara zote za uthibitisho wa mapato na matumizi ya fedha ya shughuli husika.
- vii. Kupeleka fedha zote benki za makusanyo ya Ankara za Maji kabla ya Matumizi.
- viii. Kushauriana na Msimamizi wa Jumuiya katika masuala yanayohusu fedha katika kutekeleza shuguli za mradi.

MSAHARA:

Kazi hii ni ya Mkataba na Mshahara utalipwa kutokana na Mapato/ Makusanyo ya Mauzo ya Maji kwa mradi husika chini ya Usimamizi wa Bodi ya Maji ya Mradi wa Maji katika Kijiji husika.

MAMBO YA MSINGI YA KUZINGATIWA:

- 1) Maombi yote yaambatishwe na CV(Maelezo Binafsi), Vivuli vya Vyeti vya Masomo/ Mafunzo na Vyeti vya kuzaliwa.
- 2) Muda wa kuleta maombi haya ni ndani ya siku 14 kuanzia tarehe 1/10/2020 ya Tangazo hili, siku ya mwisho kupokea maombi haya ni tarehe 14/10/2020, saa 9:30 Alasiri.
- 3) Waombaji wote waweke namba zao za simu na anuani za barua pepe (email kwa walionazo) kwenye barua za maombi, majibu yatatolewa kwa njia ya simu au barua pepe kwa wote watakaoitwa kwenye usaili.
- 4) Waombaji waweke picha moja ya rangi (Passport size) iliyopigwa hivi karibuni katika barua zao za maombi.

Barua zote za maombi ziandikwe kwa Mkono na ziwasilishwe kwa anuani:-

MENEJA RUWASA,

S.L.P 1229,

CHAMWINO,

DODOMA.

Au barua neve:chamwinodm@ruwasa.tz

**TANGAZO HILI LIMETOLEWA NA:
MENEJA WA RUWASA WILAYA YA CHAMWINO KWA NIABA YA JUMUIYA ZA
WATUMIA MAJI NGAZI YA JAMII.**